

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA
MTIHANI WA UALIMU DARAJA LA A**

680


UALIMU ELIMU YA AWALI

Muda: Saa 3

Jumatatu, 07 Mei 2018 asubuhi

Maelekezo

1. Karatasi hii ina sehemu A, B na C zenye jumla ya maswali kumi na sita (16).
2. Jibu maswali yote katika sehemu A na maswali mawili (2) kutoka katika kila sehemu B na C.
3. Sehemu A ina alama arobaini (40) na sehemu B na C zina alama thelathini (30) kila moja.
4. Simu za mkononi na vitu vyote visivyoruhusiwa **havitakiwi** katika chumba cha mtihani.
5. Andika Namba yako ya **Mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.



SEHEMU A (Alama 40)

Jibu maswali yote katika sehemu hii.

1. (a) Eleza kwa kifupi maana ya Elimu Jumuishi.
(b) Andika kwa kifupi njia tatu ambazo mwalimu wa Elimu ya Awali anaweza kuzitumia kuwatambua watoto wenye mahitaji maalum.
2. (a) Eleza kuhusu dhana ya ushirikishwaji wa wazazi katika uendeshaji wa shule ya Elimu ya Awali.
(b) Orodhesha shughuli tatu ambazo wazazi wanaweza kushiriki katika uendeshaji wa kituo cha Elimu ya Awali.
3. Ainisha changamoto nne zinazoweza kuwakabili watoto wa Elimu ya Awali zinazohitaji ushauri nasaha.
4. Orodhesha sifa nne zinazoashiria kukua kimaono kwa mtoto wa elimu ya awali.
5. (a) Unaelewa nini kuhusu kitabu cha mwongozo wa mwalimu.
(b) Andika faida tatu za kitabu cha mwongozo wa mwalimu katika kufundisha elimu ya awali.
6. Andika kwa kifupi hoja nne kuthibitisha umuhimu wa mapitio ya maandiko wakati wa kufanya utafiti katika Elimu ya Awali.
7. Orodhesha sifa nne za darasa la Elimu ya Awali.
8. Eleza kwa kifupi jinsi mbinu zifuatazo zinavyoweza kutumika katika kupata taarifa za mtoto wa Elimu ya Awali.
(a) Mahojiano
(b) Uchunguzi kwa makini
(c) Ukusanyaji wa takwimu
(d) Kutumia maono.
9. Bainisha faida nne za kufanya tathmini ya maendeleo ya mtoto wa Elimu ya Awali.
10. Orodhesha manufaa manne ya Elimu ya Awali kwa watoto wa Kitanzania.

SEHEMU B (Alama 30)

Jibu maswali mawili (2) kutoka katika sehemu hii.

11. Ainisha wadau sita wa elimu na kwa kila mmoja eleza namna anavyotumia matokeo ya tathmini ya elimu ya awali kuboresha elimu nchini Tanzania.
12. Kwa kutumia hoja sita bainisha vigezo vya mtaala wa Elimu ya Awali ulio bora.
13. Eleza bayana changamoto sita katika uendeshaji wa Elimu ya Awali nchini Tanzania.

SEHEMU C (Alama 30)

Jibu maswali mawili (2) kutoka katika sehemu hii.

14. (a) Eleza faida mbili na dosari mbili za kufundisha kwa njia ya maonesho kwa watoto wa Elimu ya Awali.
(b) Fafanua mambo mawili ya kuzingatia wakati wa kutumia njia ya maonesho katika kufundisha watoto wa Elimu ya Awali.
15. (a) Tofautisha kati ya mkoba wa kazi na orodha hakiki.
(b) Andaa orodha hakiki kwa watoto Kulwa, Doto, Masanja na Koku ukizingatia viwango vilivyofikiwa pamoja na kuonesha shughuli ndogo zinazotendwa na mtoto kuonesha umahiri wa kuhusiana.
16. Andaa andalio la somo kwa watoto wa Elimu ya Awali kwa kuzingatia umahiri mkuu wa kutunza afya na shughuli ndogo ya kufanya vitendo vinavyoonesha namna ya kufanya usafi wa nguo.